# DARASA LA TANO - MWAKA 2016
# KISWAHILI

*JINSI YA KUTUMIA HII KARATASI*

**MUDA: SAA MOJA DAKIKA AROBAINE**

*1. Tumia penseli ya kawaida*

*2. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:*

*(i) JINA LAKO (ii) JINA LA SHULE LAKO*

*3. Kwa kila jibu lako lionyeshe katika karatasi ya majibu na wala siyo katika hii ya maswali.*

***Soma kifungu kifuatayo kisha ujibu maswali.***


Hapo zamani __1__ kale. Palikuwa na mzee ___2___.ambaye alikuwa ameishi miaka___3___. Mzee huyu alikuwa mweusi___4___kama___5___. Aliishi na __6___pamoja na wanawe. Mzee Ali alikuwa na watoto sita, wasichana__7__na___8___wavulana vilevile___9___. Mke wake mama nina alikuwa amependa ___10___kama ___11___na kutembea kwa___12___ Lo! Wahenga ____13___waliponena kwamba___14___macho haambiwi ___15___.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. ka | C. za | D. na |
| 2. | A. moja | B. mmoja | C. mja | D. muja |
| 3. | A. mengi | B. mengine | C. mingi | D. nyingi |
| 4. | A. ndi | B. pepepe | C. tititi | D. pija |
| 5. | A. barafu | B. makaa | C. radi | D. theluji |
| 6. | A. muke | B. mkewe | C. mkwe | D. muvuke |
| 7. | A. tatu | B. watatu | C. mtatu | D. tupu |
| 8. | A. vile | B. pia | C. nia | D. tena |
| 9. | A. tupu | B. tatu | C. watatu | D. mtatu |
| 10. | A. kuiga | B. kuringa | C. runinga | D. kuninga |
| 11. | A. moshi | B. mosi | C. tausi | D. tanusi |
| 12. | A. mdaha | B. midaha | C. madaha | D. kidaha |
| 13. | A. hakukosa | B. alikosa | C. walikosa | D. hawakukosa |
| 14. | A. chenye | B. mwenye | C. zenye | D. wenye |
| 15. | A. atazame | B. mtazame | C. tazama | D. kutazama |

***Jibu maswali ya 16-30 kwa kufuata maagizo***

16. Kiti hiki ni changu
Viti ___ ni ___
A. vivi vyetu B. hivi vyangu
C. hivi vyetu D. hiki vyetu


17. Andika majina ya maumbo haya




A. pembetatu, mche, duara
B. duara, mche pembetatu
C. mche, duara, pembetatu
D. duara pembetatu, duara dufu

18. Malipo ya kusafiri ni___________
A. karo B. nauli
C. pesa D. mahari

19. Hili vazi huitwa_____________



huvaliwa na kina_____
A. sketi, baba B. kaptura, mama
C. kanchiri, mama D. shimizi , mama

20. Kucheza_______sikupendi
A. wake B. zake
C. kwake D. yake

21. Nguo ya bibi arusi ilikuwa_____kama_____
A. nyeusi makaa B. nyeupe pamba
C. nyekundu damu D. nyembamba sindano

22. Tumia amba kwa uangalifu.
Kinanda kilicho na wimbo
A. kinanda ambacho kina wimbo
B. kinanda ambayo ana wimbo
C. kinanda ambazo kina wimbo
D. kinanda ambalo kina wimbo

23. Andika kinyume cha
Kijana analia
A. mzee analia B. msichana analia
C. msichana anacheka D. mzee anacheka

24. Kanusha sentensi hii: Mpishi anapika
A. wapishi wanapika B. mpishi anapika
C. mpishi ananipikia D. mpishi hapika

25. Tafadhali nenda ukani____chakula nile
A. pazie B. pasie
C. pashie D. paze

26. Kuwa na usingizi mzito ni________
A. kulala fofofo B. kutazama
C. kutolala D. kuamka

27. Mtu akiona chakula kitamu yeye humeza ___
A. maji B. makamasi
C. mate D. damu

28. Andika jina la akisami hii $^3/_4$
A. robo mbili B. tatu nne
C. robo tatu D. tatu kwa nne

29. Andika tarakimu hii kwa maneno 1224



Test compiled by Schools Net Kenya, Term 1, 2016 | Available online at www.schoolsnetkenya.com
Contact details: E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 0711882227

A. elfu mbili mia mbili na nne
B. elfu moja mia mbili na ishirini
C. elfu moja mia mbili na ishirini na nne
D. elfu moja ishirini na nne

30. Mtoto wa mtoto wako utamwita_______
A. kitukuu B. kiningina
C. mjukuu D. mpwa

***Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali 31-40***

Hapo zamani za kale paliishi mama aliyekuwa na watoto mapacha yaani lila na fila. Lila na Fila walifanana kama shilingi kwa ya pili usingejua nani aliyekuwa Fila na nani alikuwa Lila. Walipozaliwa hivi baba yao aliaga dunia.

Basi watoto hawa walisomea shule ya msingi ya kilimani. Walijikaza kisabuni shuleni walitia bidii katika masomo yao kwani mama yao aliwafundisha kwamba elimu ndio uti wa mgongo wa maisha mema ya baadaye.

Walipofika darasa la saba fila alianza kutotii amri ya walimu shuleni na hata mama nyumbani. Yaani alikuwa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini lo! wahenga hawakukosea waliponena kwamba asiyesikia la mguu huvunjika guu. Aliendelea na hiyo tabia na mwishowe alikataa katakata kwenda shuleni.

Lila naye alijipiga moyo konde na kutia bidii darasani. Alijaliwa kuwa mwanafunzi bora katika taarafa na alijiunga na shule ya upili ya Ngiya. Alifunza na baadaye alijiunga na chuo kikuu cha Nairobi akaenda kusomea udaktari.

Fila naye alijiamulia kwenda kupata jiko. Alizaa watoto wengi aliishi maisha ya ufukara

Lila naye alimaliza shule akapata kazi na kuanza kumsaindia mama yake.

31. Mama huyu alikuwa na watoto
A. watatu B. wanne
C. mbili D. wawili

32. Walifanana kama shilingi kwa ya pili inamaanisha wali_____
A. fanana kidogo B. fanana sana
C. fanana nusu D. fanana mdogo

33. Kulingana na ufahamu baba ya Lila na Fila ali____dunia
A. kwenda B. oga
C. aga D. toka

34. Wahenga ni kina nani
A. vijana B. wasichana
C. wazee D. watu

35. Aliyevunjika guu katika hadithi hii ni___________
A. fila B. Lila
C. mama D. mwalimu

36. Mapacha hawa walisomea katika shule ya msingi ya______
A. mlima B. kilima
C. kilimani D. lima

37. Aliyejiunga na chuo kikuu cha Nairobi ni______
A. maa B. baba
C. lila D. fila

38. Hasikii la mwadhuni wala la mteka maji msikitini inamaanisha kwamba___________
A. hasikii mambo
B. amekufa
C. hana masikio
D. hasikii analoambiwa na yeyote

39. Aliyekuwa mwanafunzi bora katika taarafa ni______
A. fila B. lila
C. leila D. laula

40. Kichwa mwafaka cha hadithi hii ni
A. Mama mzazi
B. Bidii ya mchwa
C. Asiyeskia la mkuu huvunjika guu
D. mwenyè macho haambiwi tazama

***Soma kifungu hiki na ujibu maswali yafuatayo***

Paukwa! hapo zamani za kale paliishi hayawani wawili. Mmoja aliitwa popo na wapili aliitwa tembo. Tembo ambaye jina lake jingine ni ndovu. Hawa hayawani kila mara walibishana juu ya umaarufu wao. hakuna aliyekubali kushindwa popo alidai kuwa alikuwa maarufu kwa sababu ya ukubwa wake na nguvu nyingi.

Tembo aliketi chini na kufikiria mara tu akapata jibu. Alimwambia popo ameshindwa kwa nguvu

Baada ya ubishi mwingi, waliamua kuhakikisha popo aliishika kamba pande mmoja na Tembo upande mwingine. Kwa kweli akili ni nywele na kila mtu ana zake. Popo alifunga kamba kwenye mti uliokuwa karibu na kuchoka alichokuwa karibu nacho. Ndovu alivuruta kamba mpaka ikakatika. Alianguka chini na kuulalia mkonga wake. Hadi sasa mkonga wa ndovu unaweza kujikunja kuelekea pande zote kwa urahisi zamani. Haukuweza kujikunja.

41. Neno hayawani linamaanisha
A. popo na ndovu B. tembo
C. popo D. wanyama

42. Wanyama wangapi wametajwa katika hadithi hii
A. wawili B. wanne
C. watatu d. hatujaambiwa

43. Ni nani alikuwa mjanja
A. ndovu B. popo
C. simba D. tembo

44. Ubishi wa wanyama ulikuwa juu ya_____
A. ujanja B. uzito
C. umaarufu D. kinyonga

45. Hayawani hawa walitumia njia gani kutambua aliyekuwa maarufu
A. kuvuta kamba B. kukimbia
C. kupigana D. kuongea

46. Popo ali________
A. aliachilia kamba B. alifunga kamba kwa mti
C.alikata kamba D. ivuta kamba sana

47. Paukwa__________
A. marahaba B. karibu
C. pakawa D. paukwa sana

48. Kamilisha methali hii
Akili ni_______________
A. ali kila mtu anayo B. dama kila mtu anayo
C. maarifa kil mtu anayo D. nywele kila mtu ana zake

49. Zamani mkonga wa ndovu ulikuwa
A. haujikunji kwa urahisi B. mrefu sana
C. mwembaba D. unajikunja sana

50. Baada ya kuvuta kamba kwa mda mrefu kamba_____
A. kamba iliachiliwa na popo
B. ilirejuka
C. ilionekana
D. ilikatika